SEBHA UNIVERSITY JOURNAL OF HUMAN SCIENCES VOL.21 NO. 2 2022
DOI: 10.51984/JOHS.V21I2.1989

مجلة جامعة سبها للعلوم الإنسانية
Sebha University Journal of Human Sciences

Journal homepage: https://sebhau.edu.ly/journal/index.php/johs

# Maudhui Yanayojitokeza Katika Tamthilia Ya Kaptula La Marx Kupitia Tashtiti

*Abdallah Masoud[1], Mohamed Omary [2]

Department of African Languages, Faculty of Languages and Translation, Al-Azhar University, Egypt
Mwanafunzi wa Uzamivu wa Chuo Kikuu Huria, Dar Esalaam, Tanzania.

**Keywords:**
Fasihi
Nadharia ya Simotiki
Nadharia ya Sosholojia
Tamthilia
Tashtiti

**ABSTRACT**

Lengo kuu la makala haya ni kuchunguza maudhui ya tamthilia ya kitanzania kaptula la marx kupitia tashtit. Makala haya yanalenga kutathmini maudhui yanayojitokeza kwenye tamthilia hiyo na ni kweli kuwa tamthilia hii ina umuhimu wa kimaudhui na kifani, na inaakisi uhalisia wa mambo katika jamii katika kipindi cha muhimu kwenye historia ya nchi husika. Madhumuni mahsusi ya makala haya ni kuchambua maudhui ya tamthilia ya tajwa ili kuona hatua za maendeleo kimaudhui zilizofikiwa katika tamthilia. Data za utafiti zitakusanywa kwa kutumia mbinu ya upitiaji wa nyaraka maktabani. Na nadharia ya soshiolojia imeongoza makala haya katika uchanganuzi wa maudhui yaliyojitokeza kwenye tamthilia tajwa. Mtafiti amesoma kazi tangulizi katika maktaba za chuo kikuu huria cha tanzania, chuo kikuu cha cairo, chuo kikuu cha dar es salaam na chuo kikuu cha al-azhar. Data hizo zimechambuliwa kwa kutumia mkabala wa kimaelezo kwa madondoo kutoka katika matini ya tamthilia hiyo katika kushadadia hoja.

# قضايا مسرحية شورت ماركس من خلال السخرية

*عبد الله مسعود سعد أحمد[1] و محمد عمر ماجوو [2]

قسم اللغات الافريقية، كلية اللغات والترجمة، جامعة الازهر، مصر
قسم اللغات، كلية الدراسات الإنسانية، الجامعة المفتوحة، تنزانيا

**الكلمات المفتاحية:**
الأدب
المسرح
السخرية
النظرية الاجتماعي
النظرية السيميائية

**الملخص**

تتناول هذه المقالة القضايا الموجودة بمسرحية شورت ماركس من خلال السخرية الموجودة داخل المسرحية، كما تهدف إلى تحليل القضايا الموجودة داخل المسرحية لما لها من دور في التعبير عن قضايا المجتمع التنزاني من وجهة نظر الكاتب، كما تعكس المسرحية أنماط متعددة من القضايا داخل المجتمع في حقبة زمنية محددة. كما أنها تعكس رؤية وتطور القضايا المجتمعية المنظورة داخلها.

قام الباحثان بقراءة أولية للمسرحية للتعرف على أبرز القضايا والتطرق إلى السخرية كعنصر من عناصر البناء الفني للمسرحية، كما تم الاطلاع على الأبحاث ذات الصلة بالمسرحية أو بعنصر السخرية في المسرح السواحيلي في بعض المكتبات داخل محافظة دار السلام بتنزانيا.

اعتمد البحث على النظرية الاجتماعية لما لها من دور بارز في تحليل القضايا والظواهر الاجتماعية داخل المسرحية، وتحليل القضايا من وجهة نظر تلك النظرية واسهاماتها في التعرف على صفات وسمات المجتمع داخل المسرحية.

## Introduction

Makala haya yameshughulikia suala la tashtiti kama mbinu ya kuwasilisha maudhui yanayojitokeza kwenye tamthilia ya Kaptula la Marx. Fasihi ni kioo cha jamii kwa hivyo inatarajiwa kuibua na kuelezea hali halisi katika jamii, na fasihi ina majukumu makubwa, miongoni mwa majukumu yake katika jamii ni kuelekeza jamii na kutoa maadili, kuonya, kuelimisha, kushauri kati ya majukumu mengine. Baadhi ya waandishi wamezingatia masuala tofauti na mbalimbali ya kijamii kupitia kazi zao na wamefanya hivyo kwa kutumia fasihi (Tamthilia. Riwaya. Ushairi n.k). Fasihi ya Kiswahili hueleza mielekeo ya jamii. wengi walifanya kazi za kuchunguza

*Corresponding author:
E-mail addresses: abdallahmasoud88@gmail.com, (M. Omary)Omarymohamed36@gmail.com
*Article History : Received 26 August 2022 - Received in revised form 28 October 2022 - Accepted 01 November 2022*

tamthilia ili kuona ni kwa namna gani imebainisha hali ya jamii inahusika. Utanzu huu huandikwa kwa mtindo wa mazungumzo kama mchezo wa kuigizwa. Na bila shaka jamii yo yote ina tamaduni zao na njia zao za kuelezea hali zao. Kwa mantiki hii, ni dhahiri kuwa Watanzania wana namna yao ya kuyatazama mambo mbalimbali kutokana na mielekeo yao ya kijamii. Kutokana na hili, kuna haja ya kufanyika kwa utafiti kutathmini jinsi tashtiti inavyoibua maudhui katika tamthilia.

Wafula (1999) anaeleza kwamba tamthilia ni utungo wa fasihi unaowasilisha hadithi na migongano kwa kutumia maongezi na matendo ya wahusika. Ni ule mtungo hasa ulioandikwa kwa ajili ya kuigizwa. Na amesema pia kuwa drama ni somo linalohusu uigizaji wa hali fulani iwe ni vitendo au tabia au hisia za binadamu kwa kufuata taratibu maalum. Kwa maana kwamba utungo wa kisanaa huweka wazo fulani katika matendo na mazungumzo.

Pia, Wamitila (2003) anaeleza kuwa tamthilia ni kazi ya kidrama na ya kimaongezi ambayo huigizwa mbele ya hadhira au kazi iliyoandikwa kusomwa, kimuundo, hugawika katika matendo na maonesho, na mazungumzo huchukua sehemu kubwa katika uwasilishaji wake na maudhui. Hapa Wamitila anasisitiza kwamba tamthilia ni utungo ambao unaweza kuwa umeandikwa au haukuandikwa; kwa maana sio lazima kutendwa jukwaani. Kazi yoyote ya sanaa ikiwa tamthilia, riwaya na hadithi fupi bila shaka lazima yapo matumizi ya lugha, miongoni mwa matumizi hayo ni tashtiti/futuhi (Njogu na Chimerah, 1999). Wataalamu mbalimbali wanaeleza maana ya tashititi ambapo Wamitila (2003) anaelezea kuwa futuhi/tashititi ni dhana ya ucheshi inayotumika kuelezea uwezo wa kazi ya fasihi na sanaa ya maonyesho na kusababisha vichekesho kwa msomaji au mtazamaji.

Naye Wamitila (2002) anafasili dhana ya futuhi kwa kusema; utanzu huu huwa mwepesi ulinganishwapo na tanzia. Lengo la kimsingi ni kuchangamsha na kuishia kwa namna ya kufurahisha. Lazima tukumbuke kuwa kusema futuhi inafurahisha haina maana kuwa dhamira yake haina uzito. Wamitila (2003) anaendelea kueleza kwamba tashtiti ni mbinu ambapo mwandishi hutumia vichekesho, kinaya na dhihaka kufichua uovu fulani uliopo katika jamii au ujinga ambao umetawala katika jamii.

Kwa jumla tunaweza kusema kwamba tashititi ni matumizi ya lugha ambayo yamesheheni ucheshi ndani yake na kupitia ucheshi huo ndimo ambapo maudhui hujitokeza. Tashititi hujitokeza katika vipengele mbalimbali vya matumizi ya lugha pamoja na tamathali za semi kama tashibiha, tashihisi, sitiari, kinaya, kejeli. Dhihaka, utani, picha, taswira na ishara. Katika utafiti huu, tutaweza kuibainisha vema tashititi kupitia vipengele vya matumizi ya lugha kama ilivyotumika katika tamthiliya teule.

Highet (1962: 231) ameeleza kuwa tashtiti ni istilahi ya Kiswahili inayotokana na neno la Kiingireza “Satire” ambapo pia istilahi hii awali ilitokana na neno la Kilatini “Satura” ambalo maana yake ya kimsingi ni “tele, iliyojaa”. Baadaye satura imekuja kujulikana kwa maana ya mchanganiko uliojaa vitu mbalimbali. Kwa hiyo tashtiti inabeba maana mbalimbali kitu ambacho kinaonekana na kitu kingine haiko wazi, kwa mafano unapoona gari mbovu na unasema “Oh gari nzuri kabisa” hapo sentinsi inaonekana maana nzuri lakini kwa ndani ni tashtiti, na njia za tashtiti ni nyingi, na lengo lake ni kushusha hadhi ya vitu kwa ajili ya kukosoa jamii inahusika. Hivyo, tashtiti ni mbinu inayotumiwa na mwandishi wa fasihi kupitia vichekesho, kinaya na dhihaka huufichua uovu fulani uliopo katika jamii au ujinga ambao umetawala katika jamii (Wamitila 2003). matumizi ya tashtiti husababisha kicheko, furaha au ucheshi. Tashtiti pia ni sanaa jumuifu; yaani, hubeba kwa pamoja kejeli (kinaya), kijembe, ubezaji, na dhihaka. Kwa mara nyingine, pamoja na maelezo haya kutuelekeza katika umahususi wa dhana ya tashtiti. Na lengo la tashtiti ni kuhakiki vichekesho, pili ni kupiga picha maalum kuhusu tukio au mhusika au kundi la watu kwa njia ya vichekesho.

**Kazi tangulizi:**

Utafiti katika tamthilia na tashititi haujafanywa kwa kiasi kikubwa ikilinganishwa na uchunguzi wa maudhui katika tamthilia. Wapo watafiti wachache ambao wamefanya utafiti katika eneo la ufutuhi na tashititi hata sitiari katika baadhi ya tamthilia za Kiswahili. Ramadhan (2005) alifanya utafiti wenye anuani ya kuchunguza sitiari katika tamthilia za Mashetani na Ngoma ya Ng’wanamalundi na kubaini kwamba kuna ufanano mkubwa wa matumizi ya sitiari katika tamthilia hizi hususani sitiari zinazohusika na masuala ya uchawi na ushirikina. Kimsingi, utafiti huu umetusaidia kupata uelewa kwamba sitiari zipo za aina nyingi na sitiari zina nafasi kubwa sana katika kujenga tashititi ambazo ndizo tunazoshughulikia katika kazi hii. Naye Mrikaria (2010) anaeleza kwamba, kejeli katika fasihi ni chombo cha kuibua maovu ambayo yamejificha katika jamii ili yatambuliwe na kukomeshwa. Anaendelea kueleza kwamba, kejeli ni chombo ambacho kinatumika katika kujenga tashititi ambamo ndani ya tashititi ndimo kumefumbatwa dhamira mbalimbali zikiwemo dhamira za maovu na mambo mabaya yanayofanywa katika jamii. Utafiti wetu unakusudia kuchunguza tashititi katika tamthilia yaa Kiswahili ya Kaptula la Marx ili kuona maudhui yanayojitokeza kupitia tashtit na vipi matumizi ya tashititi katika ujenzi wa dhamira. Naye Mmata (2018) alifanya utafiti na kuandika tasinifu yenye anuani kuhusu usawiri wa mhusika kiongozi wa kisiasa katika tamthilia za Kiswahili za Kaptula la Marx na Seserumbe. Kimsingi, katika matokeo ya utafiti ilibainika kwamba kazi hizi zinawasawiri viongozi wa kisiasa kama watu ambao hawaaminiki na siku zote wapo kwa ajili masilahi yao na siyo masilahi ya wananchi wanaowaongoza. Inatolewa mifano ya namna viongozi wanavyokuwa na mali nyingi huku wananchi wao wakiwa masikini na hohehae waliojawa na ufukara. Kwa hakika, kazi hii ya Mmata (ameshatajwa) imetusiadia sana kwanza kupata uelewa wa jumla kuhusu tamthilia ya Kaptula la Marx ambayo ni kazi teule katika Makala yetu ya kuchunguza tashititi katika tamthilia. Mwanga wa uelewa ambao tumeupata utatusaidia katika kusukuma mbele makala yetu na kuweza kutimiza malengo mahususi yaliyokusudiwa.

**Mkabala wa Kinadharia:**

Makala haya yameongozwa na nadharia ya Sosholojia. Melezo ya nadharia hii yameelezwa katika sehemu hii kama ifuatavyo:

**Nadharia ya Sosholojia**

Nadharia ya sosholojia huikabili kazi ya fasihi kwa kuangali jinsi inavyohusiana na mazingira ya kijamii Msokile (1992). Wamitila (2003) anaeleza kuwa nadharia hii hutumiwa na wahakiki au wanahistoria ambao nia yao ni kuthibitisha jinsi kazi fulani ilivyoathiriwa na vitengo fulani vya mazingira kama vile tabaka la mwandishi, jinsia yake, matamanio yake, mtindo wa uwazaji, muktadha wa kiuchumi, tabaka la kijamii ya hadhira na thamani za hadhira lengwa.

Kulingana na *Encyclopaedia Britannica Online* (2011) mwasisi wa nadharia hii ni Germaine de Stael (1766 – 1817) mwanzoni mwa karne ya 19. Umuhimu wake kifasihi uliibuka katika matini zake *A Treatise of Ancient and Modern Literature* (1803) na *The influence of literature upon society* (1835). Kazi hizi zina wingi wa mawazo mapya na mielekeo mipya. Nadharia yake ya kimsingi ni kwamba, kazi ya kifasihi lazima ionyeshe uhalisi wa kimaadili na wa kihistoria, na hali ya kitamaduni, kimaadili, kiroho na kisiasa, na mitindo ya uwazaji ya taifa ambamo kazi ya kifasihi imetungwa.

*Enclopaedia Britannica Online* (2011) wanaeleza kuwa mawazo ya de Stael yalichukuliwa na Hippolyte Taine (1828 – 1893), akayaunda upya na kuyakuza. Kwa sababu hii, anachukuliwa kuwa mwasisi wa nadharia ya sosholojia ya fasihi.

Wellek na Warren (1978) wanasema kuwa, kwa kawaida fasihi huibuka ikiwa na uhusiano wa karibu na asasi fulani za kijamii. Na wanatoa rai kuwa fasihi ina uamilifu wa kijamii

ambao hauwezi kuwa wa mtu mmoja binafsi. Kwa sababu hii, maswali mengi ambayo huibuka katika uchanganuzi wa kifasihi aghalabu huwa maswala ya kijamii. Na uhusiano baina ya fasihi na jamii hujadiliwa kwa kutanguliza ufungamano wa fasihi na jamii. Wahakiki wa dhana hii wanadai kuwa ni makosa kuchukua fasihi kama kigezo cha kuashiria jinsi jamii yoyote ile ilivyo. Walidai kuwa kazi kama zile za mwandishi maarufu Shakespeare na tenzi za Milton au kazi ya Burke haziwezi kuchukuliwa kama kiashiria cha jamii zao. Jinsi mwandishi anavyowasilisha kazi yake hutegemea tajriba, uzoefu na mtazamo wake kuhusu maisha hivyo basi itakuwa si kweli kufikiri kuwa kazi ya mtu binafsi ni kiashiria cha maisha ya jamii kwa ujumla katika jamii anamotoka. Mtazamo wa fasihi kupitia sosholojia, hutufanya tumchukue mwandishi kama zao la nguvu za kisosholojia za wakati wake na kuepuka kumpunguzia sifa za ubunifu asilia.

Kulingana na James Sutherland (1957), "jinsi ambavyo mwandishi alivyoandika hutegemea kipindi alichoandika, tabaka ambamo alizaliwa, elimu aliyopokea pamoja na dini yake". Pingamizi nyingine kuhusu matumizi ya elimujamii ya fasihi ni mtazamo wa mwandishi na nguvu za kisosholojia ambazo huchunguza sehemu teule na hivyo kuufanya mtazamo wa kijumla kukosa maana. Wahakiki wanashikilia dhana kwamba uchunguzi wa fasihi unahitaji tuwe na wazo kuhusu kile ambacho ni muhimu na kile ambacho si muhimu. Wahakiki wanaopinga mbinu ya kisosholojia hawapingi kuwepo uhusiano baina ya fasihi upande mmoja na hali ya kijamii, uchumi na siasa upande mwingine. Uchunguzi wa kijamii kuhusu kazi ya maandishi au mwandishi mwenyewe utatusaidia kumchunguza mwandishi kama mwanachama wa jamii, athari za kijamii zilizomwathiri na kumpatia msukumo wa kubuni kazi ya sanaa.

Thiong'o (1978) anaeleza kuwa fasihi ina uhusiano na maisha ya kila siku ya jamii kwani haikui (fasihi) wala kuchipuka katika ombwe tupu. Anatoa rai kuwa fasihi hupewa msukumo, umbo, mwelekeo na upeo na nguvu zinazotoka katika jamii.

Njogu na Chimerah (1999) wameeleza kuhusu nadharia ya sosholojia inayofungamanisha fasihi na jamii hasa katika nchi zinazoendelea kwa sababu nadharia hii huthibitisha kuwa fasihi ni kielelezo cha ukweli uliopo katika jamii. Inasisitiza kuwa fasihi ni amali ya jamii.

Wamitila (2005) anaashiria kupendelea nadharia ya sosholojia ya fasihi kwani anasema kuwa, ni lazima kazi ya mwandishi yeyote iakisi mazingira yake, siasa ya nchi yake na mambo mengine ambayo yanamhusu. Kutokana na maelezo ya nadharia ya sosholojia ya fasihi ambayo tumeyaeleza katika sehemu hii yatatufaa katika utafiti wetu, kwa hiyo tutaitumia nadharia ya sosholojia ya fasihi kuihakiki dhamira ndani ya tamthilia teule, na kwani pia nadharia ya sosholojia ya fasihi inaweka wazi uhalisi uliopo katika jamii kwa kuyasawiri mambo vile yalivyo bila kuupendelea upande fulani.

**Muhtasari wa tamthilia ya Kaptula la Marx**

Tamthilia ya Kaptula la Marx iliandikwa na Kezilahabi na ilichapishwa mwaka wa 2010. Kaptula la Marx ni tamthilia inayohusu mabadiliko baada ya uhuru, na njia zinazotumika kwa ajili ya maendeleo. Na tamthilia imeongea pia sera ya viongozi wa Afrika baada ya uhuru.

Kezilahabi anawavalisha Rais Kapera (Mhusika mkuu) na Mawaziri makaptula ambayo yanawafanya kuwa vichekesho kwa nia ya kuonyesha kuwa vingozi hawa wa Kiafrika wanafuata falsafa ya uongozi ya Ujamaa wa Kiafrika wasiouelewa. Na Mwandishi kaonyesha kwamba viongozi hao hawajasaidi nchi hizo zilizopata uhuru. Na pia kiongozi na baraza la mawaziri wanawakandamiza wananchi hasa wapinzani wamewekwa gerezani ili hawawezi kuwasilina na wananchi na kufikisha mawazo yao kwa wengenie, na pia baadhi ya wananchi wamewekwa jela bila ya hatia.

Kaptula la Marx ni tamthilia inayotahadharisha kuwa ili kuufikia usawa, haki na demokrasia kwa walio wengi, sharti wakulima na wafanyakazi waungane ili kuwaondoa mamlakani viongozi wa aina ya Rais Kapera na mawaziri wake.

**Muhtasari wa maudhui ya tamthilia ya kaptula la Marx**

Utafiti huu ulichunguza maudhui yanayojitokeza katika tamthilia ya Kaptula la Marx. Mtafiti amejaribu kubanisha na kuchambua dhamira ambazo zinatokeza katika tamthilia Kaptula la Marx.

Kama tulivyokwishaeleza kuwa tashtiti huhusisha maneno au matendo yanayodhihaki kwa lengo la kushusha hadhi ya mtu au watu au kushusha hadhi ya wazo fulani katika jamii, kwa hiyo tunakuta anwani ya tamthilia "Kaptula la Marx" ina maana ya kiishara. Kaptula ni aina ya vazi fupi. Limetumiwa kuashiria uigaji wa mitindo ya uongozi wa kigeni. Nalo 'Marx' ni ishara ya mwanafilosofia wa Kijerumani aliyeanzisha nadharia ya umaksi ili kuonyesha uhusiano wa kisiasa na kiuchumi baina ya makundi pinzani ya mabepari na wafanyakazi. Hili lilikuwa jaribio la kuielewa jinsi jamii inavyofanya kazi.

Kwa hivyo, tashtiti imetumika kwenye anwani Kaptula la Marx ili kuashiria kwamba viongozi wanaiga filosofia ya kisiasa na kiuchumi ya Karl Marx bila kuelewa jinsi inavyotekelezwa. Hii vilevile ni sitiari fiche inayodokezea maana ya ziada ya viongozi kuthamini mawazo ya kigeni na mtindo wa utawala wa kigeni usiowafaidi raia wa jumuia ya Kaptula la Marx, yaani Tanzania.

**Tashititi Katika Dhamira Ya Ujamaa**

Ujamaa ni falsafa ya maisha ambapo jamii huishi pamoja kwa kumiliki kwa usawa njia zote za uzalishaji mali bila ya kuwepo kwa matabaka na unyonyaji baina ya wanajamii (Nyerere, 1967). Nchi ya Tanzania ilikuwa ni kinara kwa nchi nyinbgine za Afrika ambazo zilitumia falsafa ya ujamaa na kujitegemea mara tu baada ya kupata Uhuru na falsafa hiyo iliwekewa misingi katika Azimio la Arusha la mwaka 1967 na baadae kuanzishwa kwa vijiji vya ujamaa na kujitegemea (Omary, 2011). Nchi za Kiafrika zilitekeleza ujamaa kulingana na mazingira ya Kiafrika na katika Kaptura la Marx inaelezwa:

> ***Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje**: Jinsi ninavyokutazamaa! Ho Chi Minh si Ho Chi Minh, Marx si Marx! Na Mao si Mao!*
>
> ***Rais Kapera**: (Anadakiza)**…** Hiyo ndiyo siasa ya nchi hii! Siasa ya Ujamaa wa Kiafrika! Hatutangamani na nchi yoyote! Rudieni (Wote wanarudia) "Hiyo…" (uk.36).*

Kimsingi, katika dondoo hili inaonekana bayana kwamba nchi za Kiafrika zilikuwa na aina ya ujamaa ambayo ilikuwa ni tofauti na ujamaa ulioasisiwa na nchi nyingine zilizozingatia mawazo ya Karl Marx wa Ujerumani. Hata kunajengwa tashititi kama mbili hivi; tashititi ya kwanza ni kuonesha kwamba nchi za Kiafrika zilikuwa na haki ya kuwa na aina ya ujamaa ambayo inaendana na mazingira ya nchi hizo. Tashititi ya pili, inajitokeza katika kuonesha kwamba nchi za Kiafrika ziliiga falsafa ya ujamaa kutoka mataifa ya Ulaya na Uchina na mataifa hayo yakashindwa kutekeleza ujamaa kama ilivyokuwa imelengwa na waaanzilishi wa falsafa hiyo. Maelezo kwamba "Siasa ya ujamaa wa Kiafrika! Hatutangamani na nchi yoyote," ni tashititi inayoonesha kwamba nchi za Kiafrika zilishindwa kutekeleza falsafa ya ujamaa na kujitegemea na kisha kutafuta sababu ya kujitetea.

Kwa hakika, tashititi zote mbili zinajenga mantiki na kwa kurejelea nadharia ya Sosholojia tunaona kwamba ni kweli mazingira ndiyo ambayo hufanya jamii moja kuchukuwa jambo fulani kutoka kwa jamii nyingine na kisha kulitengeneza jambo hilo katika muktadha wa jamii husika na kulitekeleza. Hivyo, tashititi hiyo inatoa dhamira kwamba, falsafa ya ujamaa ili iweze kutekelezwa vizuri ni lazima iwekwe katika misingi na mazingira ya nchi za Kiafrika. Mazingira na utamaduni wanchi za Kifrika ni tofauti kabisa na nchi za Ulaya na hivyo kuchukuwa falsafa ya ujamaa kama inavyotekelezwa katika nchi za Ulaya na kuileta hivyo hivyo katika nchi za Kiafrika isingeliweza kutekelezwa vizuri.

Mintaarafu ya hayo, tashititi ile ya pili ya kwamba nchi za Kiafrika zimechukuwa falsafa ya ujamaa na kuiweka katika mazingira yake lakini bado ilishindwa kutekelezwa vizuri kama ilivyokusudiwa. Pamoja na ukweli kwamba nchi za Kiafrika zilionekana kutekeleza ujamaa kwa namna yake, lakini haikueleweka vizuri na ndio maana ya maneno "Jinsi ninavyokutazamaa! Ho Chi Minh si Ho Chi Minh, Marx si Marx! Na Mao si Mao!" Hivyo, pamoja na mambo mazuri ya ujamaa lakini siasa za ujamaa zilishindwa nguvu na ubepari na mpaka hivi sasa hakuna nchi ya Kiafrika ambayo inatekeleza siasa hizo.

**Tashititi katika Dhamira ya ukosefu wa Usawa**

Usawa katika jamii ni miongoni mwa dhamira kongwe ambayo inajitokeza katika kazi nyingi za fasihi andishi na pia fasihi simulizi (Kombo, 2014). Usawa ni suala la haki ambalo limepewa nafasi kubwa katika jamii kupitia katiba za nchi husika pamoja na maazimio mbalimbali ya kitaifa na kimataifa (Shivji, 2002). Katika tamthiliya ya Kaptula la Marx tunaona dhamira ya kukosekana kwa usawa katika jamii ikijitokeza katika tashititi kama ifuatavyo:

> ***Korchnoni Brown**: Mtakwenda! Halafu mtapinda, mtapinda tena, halafu tena mtapinda. Mwishowe mtapindapinda hadi mtakapofika mabonde yenye matope. Mtapita katikati ya matope. Halafu milima, halafu misitu yenye miiba hadi mtakapofika jangwani. Kutoka jangwani mtaingia tena bondeni chini kwa chini hadi baharini. Hakuna mitumbwi wala ngalawa. Mtaogelea, ingawa kuna papa wengi. Mkishavuka mtafika nchi iitwayo Svoboda. Kabla…(uk.30).*

Dondoo hili linaonesha namna ilivyokuwa ni suala gumu kuwa na usawa katika jamii. Kuufikia usawa ni safari ndefu sana ambayo imetawaliwa na kila aina ya dhiki. Ugumu wa safari unaoelezwa hapa ndiyo ugumu wa kufikia usawa katika jamii. Hapa inajengwa tashititi ambayo ndani yake mna dhamira kuntu lakini kubwa ikiwa ni namna wananchi wanaishi katika maisha magumu yasiyokuwa na usawa katika maeneo mbalimbali na hapa eneo linaloonekana bayana ni miundombinu. Ni jambo la kawaida katika maeneo ya vijijini kuwa na barabara mbovu ambazo hazipitiki katika majira yote na wakati wa masika hali huwa mbaya zaidi. Wakati hali ikiwa hivyo katika maeneo ya vijijini sehemu kubwa ya maeneo ya mijini hali ya miundombinu huwa si mbaya bali ni afadhali kidogo. Hapa ndipo usawa unapokesekana katika miundombinu baina ya mijini na vijijini. Tumeona katika nchi ya Tanzania kwa mfano, serikali imefanya jitahada kubwa ya kuhakikisha kunakuwa na usawa katika eneo hilo la miundombinu baina ya mijini na vijijini kwa kuanzisha Wakala wa Ujenzi wa Barabara mijini na vijijini (TARURA) na kupangiwa bajeti ya kutosha katika mwaka wa fedha wa 2021/2022 na 2022/2023 (SJMT, 2022).

Na pia mwandishi kaonyesha kwamba nchi za kiafrika ni vigumu kufika kwa usawa na uadilifu kupitia mhusika Jitu (Korchnoi Brown) anaewaambia Rais Kapera na Mawaziri kuwa:

> ***Jitu:** ...sidhani kama mtafiki huko wakati wa uhai wenu. Hata robo tu ya njia bado! (Uk. 29).*

Hii ni tashititi ambayo ni muendelezo wa kile ambacho kimejadiliwa hapo juu, ikiwa na maana kwamba bila mipango madhubuti haiwezekani jamii kufikia katika usawa wa kweli katika mambo mbalimbali. Tumeona serikali za mataifa mbalimbali ya Kiafrika yakifanya jitihada katika kufikia usawa katika nyanja mbalimbali kama vile elimu, afya, maji, miundombinu, jinsia nakadhalika ambapo sera na mipango ipo na inafanya kazi vizuri. Tashititi hii pamoja na mambo mengine inawakatisha tamaa viongozi na wananchi kwamba siku moja wanaweza kufikia katika usawa wa kweli lakini inavyoonekana ni kwamba hawawezi kufikia katika usawa huo unaokusudiwa. Mara nyingine kutiana moyo ni njia ya kuhakikisha maendeleo yanapatikana na usawa katika jamii unafikiwa.

**Tashititi katika Dhamira ya Ufisadi**

Ufisadi ni dhamira jadiliwa katika kazi za fasihi na pia katika tahakiki na utafiti katika kazi hizo. Ufisadi ni kitendo cha mtu au kikundi cha watu kujipatia mali kwa njia ambayo si sahihi au kutumia madaraka na mamlaka aliyonayo katika kujipatia mali isivyokuwa halali (Bulaya, 2010). Katika kuonesha namna ufisadi ni tatizo na unapaswa kukomeshwa katika jamii, serikali mbalimbali duniani zimeanzisha vyombo vya kuzuia na kupambana na rushwa na Tanzania ni miongoni mwa nchi hizo ambapo kuna Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa. Katika tamthiliya ya Kaptura la Marx tunaona mwandishi akisawiri dhamira ya ufisadi kupitia tashititi kama ifuatavyo: Mwandishi katumia "mchezo ndani ya mchezo" mahakamani ili atumie tashtiti kwa ajili ya kuonysha ufisadi nchini. Ufisadi huu ni kuwatesa wanyonge peke yao wakati matajiri ambao wanaiba hawaulizwi. Wafungwa wanatumiwa kiishara kuonyesha kuwa haki kwenye mahakama haitekelezwi.

> ***Mfungwa 4:** … Huyo ndugu anashtakiwa kwa kosa la kuiba mkate kwenye duka la Mhindi.*
> ***Mfungwa 6**: Unakiri kosa?*
> ***Mfungwa 2**: ndiyo, lakini nilikuwa na njaa.*
> ***Mfungwa 6**: Jela miaka kumi na viboko 25.* (uk.24).

Hapo juu tunaona kwamba mtu aliyeshtakiwa kwa kuiba mkate kwenye duka la Mhindi kwa sababu ya njaa, anafungwa miaka kumi na viboko 25, na kwenye mfano mwengine hapo chini tutaona kwamba mshtakiwa mwengine kaiba pesa za shirika la ndege, kiasi cha shilingi milioni ishirini na moja akafungwa jela kwa muda wa siku moja.

> ***Mfungwa 1**: Huyo anashtakiwa kwa kosa la kuiba pesa za shirika la ndege, kiasi cha shilingi milioni ishirini na moja!*
> ***Mfungwa 6**: Unakiri kosa!*
> ***Mfungwa 3**: Ndiyo, nakiri.*
> ***Mfungwa 6**: Jela kwa muda wa siku moja!* (uk.25).

Katika madondoo mawili tumeona katika dondoo la kwanza mtu aliyeiba mkate kwa sababu ya njaa amehukumiwa kifungo cha miaka kumi na viboko ishirini na vitano. Kwa upande mwingine, mtu ambaye ameiba fedha za shirika la ndege kiasi cha milioni ishirini yeye anafungwa jela kwa siku moja tu. Hii kwa hakika ni tashititi ambayo inaonesha kukithiri kwa ufisadi katika jamii. Kwanza kuna ufisadi wa kuiba mali ya umma ambayo ni fedha ya shirika la ndege lakini pia kuna ufisadi mwingine wa watoa haki kutotenda haki kwa sababu ya ufisadi wa kupokea rushwa. Kwa kurejelea msimbo wa kimatukio wa nadharia ya Simiotiki tunapata kuiona vizuri tashititi ikijitokeza katika matukio yote mawili lile la kuiba mkate na hili kuiba milioni ishirini pamoja na hukumu iliyotolewa. Hakuna uhalisia katika matukio haya mawili jambo linaloashiria kwamba ufisadi umekithiri katika jamii kwa kiasi kikubwa.

Kwa mujibu wa nadharia ya Sosholojia, inatufunza kwamba, mara nyingi mtu mnyonge katika jamii ndiye ambaye huonewa na kunyongwa zaidi kuliko yule ambaye ni tajiri. Katika hali ya kawaida mtu ambaye amekosa chakula na kufikia hatua ya kuiba chakula, alipaswa kutazamwa vizuri na kusaidiwa kuliko kufungwa kifungo cha miaka kumi jela na viboko ishirini na vitano juu. Hapa kuna tashititi nzito ambayo inawataka viongozi na wanajamii kwa jumla kulitazama jambo hili kwa jicho la umakini zaidi ili kuwasaidia wananchi kutatua changamoto zinazowakabili badala ya kuwaongezea matatizo zaidi. Hivyo, katika dondoo tajwa hapo juu tunaona mahakama ikitajwa kitashititi kushuka kihadhi kwa kutotimiza wajibu wake ipasavyo.

**Tashititi katika Dhamira ya Ukoloni Mamboleo**

Ukoloni mamboleo ni hali ya nchi moja kutawaliwa na nchi nyingine

kifikira, kiuchumi na kiutamaduni na kuachiwa kuwa na uhuru wa kisiasa pekee ambao hujulikana kama uhuru wa bendera (Mpangala, 1997). Nchi za Kiafria zilitawaliwa na mataifa mbalimbali ya Ulaya kuanzia mwaka 1884 baadaye kupatiwa uhuru kuanzia miaka ya 1960 na kuendelea. Uhuru uliotolewa ulikuwa ni wa bendera kwa sababu nchi hizo bado zimeendelea kutawaliwa kupitia ukoloni mamboleo. Katika tamthiliya ya Kaptura la Marx mwandishi ametumia tashtiti ili kuonyesha ukoloni mamboleo kupitia taasisi kama 'Benki ya Dunia' na kaonyesha kwamba Wazungu wanazitumia taasisi hizo ili kuzikandamiza nchi za Kiafrika, kwa kudaiwa na kulimbikiziwa madeni yasiyolipika, na hiyo ndio ni ukoloni mamboleo. Tuone dondoo lifuatalo:

> ***Mfungwa 6****: Lo! Si Wazungu hao! Wengi ajabu!*
> ***Mfungwa 1****: Labda Waisraeli!*
> ***Mfungwa 6****: Mmoja wao kama Hitler! Haikosi ni ndugu yake! Wote wameenea mikoba ya fedha! Mikoba yao imeandikwa, "Benki ya Dunia!"*
> ***Mfungwa 2:*** *Wanaletea fedha au wanakuja kuchukua! Watazameni vizuri. Wameshibashiba kidogo au wana njaa!*
> ***Mfungwa 6:*** *Matumbo yamevimba, lakini meno yao yako nje kama mbwa vichaa wenye njaa!*
> ***Mfungwa 1****: Basi hiyo ni shibe ya ugonjwa!*
> ***Mfungwa 6****: Ala! Huko nje naona jela nyingine tena!*
> ***Mfungwa 1****: Kumbe wafungwa tuko wengi ulimwenguni.*
> ***Mfungwa 6****: Tena jela hiyo imeyoandikwa "Soko la Dunia!" (uk. 6:7).*

Kwenye muktadha huu Wazungu wanaowakilisha 'Benki ya Dunia' na 'Soko la Dunia' ni ishara ya ukoloni mamboleo ambao unadhibiti uchumi na biashara ya nchi za Afrika. Nchi hizi zinaingia katika jela ya kudaiwa na kulimbikiziwa madeni yasiyomalizika. Wazungu wanaorejelewa hapa wamevimba matumbo na meno yao yako nje kama mbwa vichaa wenye njaa ili kuashiria tamaa waliyo nayo. Mbwa vichaa wenye njaa ni tashititi kwamba Wazungu ni wanyonyaji wa nchi za Kiafrika kama vile mbwa kichaa walivyo hatari kwa binadamu.

Kimsingi, kwa kurejelea nadharia ya Simiotiki kupitia msimbo wa kiishara kwamba kunajengwa tashititi ya kuonesha namna benki ya dunia inavyotumia njia ya kuzikopesha nchi za Kiafrika kwa riba kubwa kiasi cha nchi hizo kulipa fedha nyingi na zenyewe na watu wake kubakia katika lindi la umasikini. Mikopo inayotolewa inalipwa karibu mara mbili ya fedha ya mkopo hali inayozifanya nchi za Kiafrika kuzidisha kukopa na kuzidi kutumia rasilimali za nchi kulipia riba ya mikopo. Soko huria linalotajwa, linatumika kunufaisha zaidi nchi zilizoendelea kuliko nchi masikini kwa sababu hizo ndizo zinazopanga bei ya bidhaa. Nchi za Kiafrika zinaweza kuwa zimezalisha bidhaa kwa gharama kubwa lakini bidhaa hizo zinapofika kwenye soko la dunia zinapangiwa bei na kuuzwa kwa bei ya chini. Vilevile, bidhaa za mataifa hayo yaliyoendelea zinanufaika na soko huria kwa sababu wanayo nishati na teknolojia ya kuzalisha bidhaa nyingi kwa gharama nafuu ikilinganishwa na nchi zinazoendelea nyingi zikiwa ni kutoka Afrika. Kwa minajili hiyo suala la ukoloni mamboleo linaendelea kuzitafuna nchi za Kiafrika na kuziacha katika umasikini usiomithilika.

**Tashititi katika Matumizi Mabaya ya Madaraka**

Madaraka ni dhamana wanayopewa baadhi ya wanajamii ili kuongoza wananchi wenzao katika kusimamia serikali na rasilimali za taifa ili ziwanufaishe wananchi wote. Utaratibu wa matumizi ya madaraka umeelezwa na kuanishwa vizuri katika katiba ya nchi, sheria, kanuni, miongozo na taratibu mbalimbali za kuongoza nchi. Katika nchi yenye kufuata sheria katika kuongoza, hatazamiwi kuona kiongozi au viongozi wakitumia madaraka yao vibaya (Msuya na Lupokela, 2010). Katika jamii kuna viongozi mbalimbali katika serikali kuu, serikali za mitaa, taasisi, mahakama, bunge, mashirika ya umma, makala wa serikali na mashirika na taasisi zisizo za kiserikali. Tuone mfano ufuatao:

> ***Mfungwa 1****: ….. Huku nje ni fujo tupu, Hali ni mbaya Zaidi kuliko ile tuliyoiacha. Watu wanakula mali ya umma ovyo! Rushwa imeshamiri! Viongozi na wakuu wa nchi wamezungukwa na mawaziri wanafiki na wabunge wenye njaa na uchu wa mali. Kaptula La Marx lavaliwa mbwembwe; watu wanateswa na kunyongwa ovyo bila hata kufikisha kortini…….. sina mengi zaidi. Labda jambo moja. Leo jioni kuna mpira kati ya mawaziri na wabunge. Nitahudhuria.(uk. 40)*

Dondoo hili linataja baadhi ya viongozi katika jamii ambao ni mawaziri na wabunge ambapo inajengwa tashititi kwamba wameshindwa kutimiza wajibu wao vizuri na kutumia madaraka yao vibaya badala ya kushauri na kuisimamia serikali itekeleze wajibu wake. Wanatajwa kuwa ni watu wenye uchu wa njaa na mali jambo linaloashiria kwamba wanatumia vibaya madaraka yao. Badala ya kutumia madaraka waliyopewa na katiba katika kuwatetea wananchi, wao wanatumia madaraka waliyopewa kujinufaisha wao wenyewe. Kwa mujibu wa nadharia ya Sosholojia, inaelezwa kwamba binadamu mara nyingi ni kiumbe ambaye hujifikiria yeye binafsi kwanza kabla hayamfikiria mtu mwingine. Hata hivyo, unapopewa kazi ya umma ni lazima umma ndiyo uwe kipaombele cha viongozi kwa sababu viongozi hao wanatumia mali ya umma katika kutekeleza majukumu yao na pia katika kulipwa mishahara na marupurupu mengine.

Katika dondoo hapo juu, kunajengwa tashititi nyingine kwamba viongozi hao tajwa hawana jambo la msingi ambalo wanaweza kusaidia wananchi kuondokana na adha na kero mbalimbali ambazo wanakabiliana nazo katika maisha ya kila siku na kucheza mpira ndilo jambo ambalo wanaweza. Hii ni tashititi ambayo inaonesha kwamba, viongozi hawashughuliki na mambo ya msingi ya kuwainua wananchi kiuchumi bali wanashughulika na mambo ambayo si ya msingi. Hivyo, wananchi wanaonekana kukata tamaa na kusema ni bora kwenda kutazama mpira kati ya wabunge na mawaziri badala ya kuwasikiliza wakitoa hoja na kujibu hoja bungeni.

Pamoja na ukweli ambao upo katika tashititi na dhamira iliyowasilishwa, bado ni ukweli pia, wapo wabunge na mawaziri ambao ni wachapakazi sana na wanatendea haki nafasi walizopewa za kuwahudumia na kuwaongoza wananchi. Maendeleo ambayo yamefikiwa katika nchi nyingi za Kiafrika Tanzania ikiwemo ni ishara tosha kwamba nchi hizo zina viongozi makini ambao wanasaidia serikali katika kutimiza wajibu wake vizuri zaidi. Pale viongozi wakuu wa nchi wanapokuwa hawaridhishwi na utendaji kazi wa baadhi ya mawaziri huwatoa katika nafasi zao na kuwateua wengine. Kwa upande wa wabunge, wananchi huacha kuwachagua kwa awamu nyingine baadhi ya wabunge ambao wanaonekana kutotimiza wajibu wao ipasavyo.

Na pia mwandishi wa *Kaptula la Marx* ameonyesha udhalilishaji wa mawaziri kupitia raisi, na maneno yanayofuata yanaashiria kejeli.

> ***Rais Kapera:*** *Una ulimi wa nyoka? Lamba pua yako basi! (Waziri anapiga magoti akiomba radhi). Lamba pua yako! (Waziri anajaribu. Ulimi unakaribia lakini anashindwa. Udende unamtoka). (uk. 11)*

Maneno ya hapo juu yanaonyesha hali ya uhusiano mbaya baina ya Raisi na waziri wake na lugha inayotumika ni ya dharau, na inaonyesha matumizi mabaya ya madaraka na udufu wa kimawazo wa viongozi walio mamlakani. Katika hali ya kawaida kiongozi mkubwa anapozungumza na kiongozi wa chini yaani msaidizi wake hutumia lugha ya staha na si lugha ya kifedhuli kwa sababu kufanya hivyo ni kutumia vibaya madaraka. Viongozi wa aina hii mara nyingi hifika mahali na kukosa watu wa kufanya nao kazi na hivyo kuchelewesha maendeleo kwa wananchi. Nadharia ya Simiotiki kupitia msimbo wake wa kimatukio, inatuambia hapa kwamba, tukio hili linashusha hadhi ya viongozi wote wawili yaani

yule anayetukana na yule anayetukanwa. Mambo kama haya hufanywa na vyombo husika vya kusimamia maadili pale kiongozi anapokosea na siyo kudhalilishwa kwa kejeli na dharau.

Katika jamii wapo baadhi ya viongozi ambao hushindwa kutimiza wajibu wao kama viongozi na kuikosesha jamii maendeleo kwa sababu ya matumizi mabaya ya madaraka lakini katika kujitetea huwasingizia viongozi waliotangulia kabla yao. Dondoo hapa chini linathibitisha kama ifuatavyo:

> ***Rais Kapera:*** *(Kwa masikitiko) Safari yote tuliyofanya, bure! Labda tulishindwa kufika kwa sababu waliotangulia walikuwa wamekwisha-haribu njia!. (uk. 37).*

Mwandishi ametumia tashtiti kuonyesha namna viongozi wa aina ya Rais Kapera, wanaposhindwa kuongoza nchi vizuri, huwalaumu viongozi waliowatangulia. Pia ameonyesha kwamba Rais Kapera, Mawaziri na Mkulima wamesafiri ili kutafuta faida kwa nchi yao kupitia kuiga nchi nyingine na mwishone safari ina madhumuni mema lakini haina faida yoyote. Matumizi ya mambaya ya madaraka huwafanya baadhi ya viongozi kuwa na mipango na maamuzi ambayo si mazuri kwa ajili ya maendeleo ya wananchi na badala yake huwa na maamuzi ya kibinafsi ambayo husababisha wananchi kutopata maendeleo. Kitendo cha kiongozi kufanya safari ambazo hazina tija na faida kwa wananchi ni tashititi inayojengwa kuonesha matumizi mabaya ya madaraka. Nadharia ya Sosholojia inaeleza kwamba, ushirikishwaji wa viongozi wote pamoja na wananchi katika maamuzi ni njia sahihi ya kufikia maamuzi yenye tija kwa taifa na ndiyo matumizi mazuri ya madaraka ya viongozi.

**Tashititi katika Dhamira ya Ukosefu wa Demokrasi**

Demokrasia ni hali ya wananchi kuwa na uhuru wa kuchaguwa viongozi wao kwa njia ya uchaguzi wa huru na haki na kuwapatia mamlaka ya kuongoza serikali (Khalifa, 2013). Kimsingi, kuna demokrasia ya moja kwa moja na kuna demokrasia ya kuchaguwa wawakilishili ambao ndiyo huingia katika vyombo vya maamuzi kwa niaba ya wananchi waliowachagua. Katika tamthiliya ya *Kaptula la Marx* mwandishi ametumia tashtiti kuonyesha ukosefu wa demokrasi kupitia kupima kiwango cha mwamko wa kisiasa *katika jamii*, na hapa tuone dondoo lifuatalo:

> ***Rais Kapera:*** *… Nina wasiwasi sana na msimamo wa watu waishio katika nchi hii! Watu hawana msimamo! (Akionyesha faili iliyo mikononi mwa waziri) Waziri wa mambo ya ndani ameniletea ripoti akieleza kuwa mwamko wa kisiasa ni mdogo sana miongoni mwa wananchi. (Akimkazia macho Daktari) Daktari! Nataka upime mwamko huu wa kisiasa. Tarisha atakuletea sampuli sasa hivi! (uk. 44).*

Dondoo hili lina tashititi ndani yake ambapo katika uhalisia kiongozi huyo anayeitwa kwa jina la rais Kapera ni mtu ambaye hapendi demokrasia lakini hapa anajifanya kusikitishwa na wananchi wake kutokuwa na mwamko wa kisiasa. Hii ni ishara kwamba, wapo baadhi ya viongozi katika jamii ambao kazi yao kubwa ni kupinga demokrasia kwa kutokuwapatia wananchi wao uhuru lakini viongozi hao hugeuka na kujifanya wao ni wapenda demokrasia. Katika uhalisia, demokrasia hushamiri na kustawi mahali ambapo imewekewa misingi ya kushamiri. Mahali ambapo demokrasia haijapewa nafasi haiwezi kamwe kushamiri na hivyo ni jambo la ajabu kuona kiongozi mkuu anashangaa watu wake kutokuwa na mwamko wa masuala ya siasa na demokrasia.

Na hapa chini pia mwandishi katumia tashtiti ili kuonyesha kwamba nchi zote za Kiafrika hazina democracy.

> ***Mfungwa 4:*** *Mimi nisingejali kutawaliwa na nchi ya Jirani. Serikali za Kiafrika ni zile zile za watawala wa Maisha. (uk.3)*

Suala la viongozi kutawala kwa muda mrefu bila kuwapatia wananchi demokrasia ya kuchagua viongozi wanaowapenda kila baada ya muda maalumu ni ishara ya kukosekana kwa demokrasia katika baadhi ya nchi za Afrika. Hapa kunajengwa tashititi ya kwamba kuna nchi bado viongozi wake hawajakubali kuwa na demokrasia ya kweli ya vitendo bali ya maneno tu. Hata hivyo, kwa sasa zipo nchi nyingi sana za Kiafrika ambazo zimeingia katika mifumo ya kidemokrasia na wananchi wanapata fursa ya kuchagua viongozi wao na pia kila mwananchi mwenye kupenda kugombea nafasi fulani ya uongozi anapata fursa ya kugombea bila kipingamizi.

**Tashititi Katika Dhamira ya Ubaguzi**

Dhamira ya ubaguzi husawiriwa kwa namna tofauti tofauti katika kazi za fasihi, ikiwa ni ubaguzi wa rangi, kimadaraka, kitabaka, kidini, kimaeneo, kielimu na kikabila kutaja kwa uchache. Wapo watu katika jamii ambao huabudu sana ubaguzi kwa kuwadharau watu wengine kwa kuwaona kuwa si lolote wala chochote. Tuone mfano katika dondoo hapa chini:

> ***Rais Kapera:*** *(Akitingisha kichwa) Kazi nzuri, kazi nzuri! (Kimya.) Vipi wale panya tuliowaweka huko jela?*
> ***Waziri wa Mambo ya Ndani:*** *Kwa muda wa miaka tisa iliyopita hatujawaruhusu kutoka nje. Habari nilizo nazo ni kwamba akili zao zinaanza kuwa butu. Hawawezi kufikiri. (uk.13).*

Matumizi ya 'panya' katika dondoo hili ni ya kitashtiti ili kushusha hadhi ya wafungwa na wapinzani waliopo magerezani ambao wamefungwa kwa amri ya raisi aliyepo madarakani. Kiongozi huyu ametumia madaraka yake kuwafunga wapinzani wake na baada ya kuwafunga anaita 'panya' ambapo ni ubaguzi wa hali ya juu. Hii pia, ni tashititi ambayo inaonyesha namna kiongozi huyo alivyolewa na madaraka mpaka anawaita wananchi wake kwa jina la 'panya'. Kwa mujibu wa nadharia ya Simiotiki katika msimbo wa kiurejelezi tunaona hapa thamani ya binadamu imeshushwa sana kiasi cha kulinganishwa na panya. Huyu ni mnyama mharibifu wa mazao, nguo na hata kula vifaranga vya kuku jambo linalofanya achukiwe mno katika jamii. Adhabu yake huwa ni kifo pale anapokamatwa au anapobainika kuwepo katika nyumba. Hivyo, kitendo cha kiongozi mkuu rais Kapera kuwaita wapinzani wake 'panya' ni ishara kwamba yupo tayari kuhakikisha wanakufa na afanywavyo panya. Katika dondoo jingine hapa chini inaelezwa kwamba:

> ***Mkulima:*** *(Akinung'unika) Hii njia mnayonipitisha mimi siijui na mimi sijui mnanipeleka wapi!*
> ***Rais Kapera:*** *Mimi ndiyo dira yenu. Aniaminiye hatapotea.*
> ***Waziri wa Mambo ya Nchi za nje:*** *Wewe ndiye haki! Wewe pekee ndiye unayeweza kufikiri. (uk. 28).*

Dondoo hili pia lina matumizi ya tashititi yenye kujenga dhamira ya ubaguzi ambapo mtu mmoja anajiona yeye ni bora kuliko watu wengine katika jamii. Katika hali ya kawaida kuona kiongozi ambaye anajielezea kuwa yeye ndiyo kila kitu katika maisha ni ubaguzi wa hali ya juu sana. Kiongozi anapaswa kutumia maarifa yaliyopo kwa wananchi wake wote ili kuliletea maendeleo taifa lake. Kiongozi ambaye anajiona yeye ni bora kuliko watu wengine ni kiongozi mbaya ambaye ana damu ya kibaguzi na taifa lake haliwezi kupata maendeleo kwa sababu litakuwa linaendeshwa kwa kutumia mawazo ya mtu mmoja tu. Ukweli ni kwamba, mtu mmoja tu hawezi kufahamu kila kitu bali hfahamu mambo machache tu na anapounganisha na mawazo na ujuzi wa watu wengine katika jamii hapo ndipo mawazo kuntu hupatikana na utekelezaji wake huzaa maendeleo. Maneno, 'Mimi ndiyo dira yenu' na 'Wewe pekee ndiye haki,' yametumika kisitiari kama ishara kwamba, Rais Kapera ndiye kiongozi anayejua njia wapasayo kuiendea ili kuufikia usawa, ukweli, haki na demokrasia.

**MAREJELEO**


1. Bakharessa S. K., (1996) *Kamusi ya Maana na Matumizi*, Nairobi, Kenya, oxford University press.
2. Brtoncini E., (1989) Outline of Swahili literature; Prose, Fiction and Drama, E.J.Brill.
3. Didas, M. (2019), "Usawiri wa Mwanamke katika Tamthiliya ya Kimfumojike: Mifano kutoka Mama Mtakatifu na Kivuli kinaishi, Tasinifu ya Uzamili ya Chuo Kikuu cha Nairobi.
4. Ireri Mbaabu, (1985) *New Horizons in Kiswahili: Asynthesis in Developments Research and Literature.* Nairobi: Bureau, first published.
5. *Highet, G. (1962) The Anatomy of Satire. Princeton: Princeton University Press.*
6. *Kayombo, P. (2019), "Sitiari katika Tamthiliya za Emmanuel Mbogo," Tsinifu ndogo ya Shahada ya Kwanza ya Kiswahili ya Chuo Kikuu cha Ruaha.*
7. Kimani wa Njugo na Rocha Chimerah, (1999) *Ufundishaji Wa Fasihi*, Nairobi, Kenya, Jomo Kenyatta Foundation.
8. Mapunjo, G. C. (2014). *Usawiri wa Mwanamke Kama Kiongozi Katika Tamthiliya: Uchunguzi wa Kivuli Kinaishi na Nguzo Mama*. Tasinifu iliyowasilishwa kwa Ajili ya Shahada ya Uzamili ya Fasihi ya Kiswahili (Haijachapishwa). Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.
9. Ramadhani, D. (2005). *The Uses of Metaphors in Mbogo's Ngoma ya Ng'wanamalundi and Hussein's Mashetani*. A Stylistic Comparison.Tasnifu ya Umahiri, (Haijachapishwa) University of Dar es Salaam.
10. Richard M. Wafula, na Njogu Kimani, (2007) *Nadharia za uhakiki wa fasihi*, Nairobi, Kenya, Jomo Kenyatta Foundation.
11. Richard M. Wafula, (1999) *Uhakiki wa Tamthilia, Historia na Maendeleo Yake,* Nairobi, Kenya; Jomo Kenyatta Foundation, Chapa ya kwanza.
12. Ponera, A. S., (2014) *Utangulizi wa Nadhalia ya Fasihi Linganishi*, Dar es Salaam, Tanzania, Karljamer Print Technology.
13. Saifu D. Kiango, (1982) *Tamthilia za Kiswahili: Dhamira Chapwa na Usuli katika Uchapwa*, Kiswahili Jarida la taasisi ya uchunguzi wa Kiswahili, chuo kikuu cha Dar Es Salaam, juzuu 49\2.
14. Semzaba, E., (2003) *Tamthiliya ya Kiswahili*. Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, Dar es salaam. Tanzania.
15. Senyamanza, C., (2014) *Misingi ya Kazi za Kubuni: Nadharia, Mbinu na Mifano ya Kazi Bunilizi*, Dar es Salaam: Karljamer Print Technology.
16. Wamitila K.W., (2003) *Kamusi ya Fasihi Istilahi na Nadharia*, Nairobi, Kenya, focus books.
17. -------------------,(2010) *Kanzi ya fasihi, Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi,* Vide-Muwa Publishers Limited, chapa ya pili.
18. --------------------,(2012) *Kichocheo cha Fasihi, Simulizi na Andishi*, Focus Book, chapa ya saba.
19. ----------------,(2002) *Uhakiki wa Fasihi, Misingi na Vipengele Vyake*, Phoenix Publishers Ltd, chapa ya kwanza.
20. *Wa Thiong'o, Ngugi. (1995). Decolonising the mind: The language of literature in Afrika. London: Curey Publishers.*
21. Wellek, R na Warren, A. (1948), *Theory of Literature*, New York, Harcourt, Brace and Company.
22. Hussein, E. (1983). "*Hatua Mbalimbali za Kubuni na Kutunga tamthilia Kufuatana na Misingi ya Ki – Aristotle*". Katika Makala za Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili. Dar es Salaam. TUKI. Kur. 197– 205.
23. Kiango, S. D. (1973). "*Maendeleo ya Fasihi ya Kiswahili Upande wa Michezo ya Kuigiza"*. Katika Kiswahili, Juz. Na. 2: 88 – 97.
24. Mlaga, K.W. (2017). *Misingi ya Ufundishaji na Ujifunzaji wa Fasihi*. Dar es Salaam: Heko Publishers Limited.
25. Mulokozi, M. M. (1996). *Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili*. Dar es Salaam: Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.
26. _______(2017). *Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili*. Dar es Salaam: KAUTTU.
27. Mutembei, A. K. (2006). "*Nadharia ya Fasihi Simulizi na Maendeleo katika Sayansi na Teknolojia"*. Katika Mulika Juz. Na. 27: 1-17
28. Njogu, K. na Wafula, R. M. (2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.